TANGAZO LA SERIKALI Na. 51M la tarehe 28/1/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE RIBA ITOKANAYO NA MIKOPO KUTOKA TAASISI ZA KIFEDHA ZA KIGENI KATIKA MRADI WA UANZISHAJI WA KIWANDA CHA KUTENGENEZA MABATI WA KAMPUNI YA LODHIA STEEL INDUSTRIES YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye Riba Itokanayo na Mikopo kutoka Taasisi za Kifedha za Kigeni katika Mradi wa Uanzishaji wa Kiwanda cha Kutengeneza Mabati wa Kampuni ya Lodhia Steel Industries ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 11 Oktoba, 2024.

Msamaha

**2**. Kodi ya zuio inayopaswa kulipwa na Kampuni ya Lodhia Steel Industries katika riba itokanayo na mikopo kutoka tasisi za kifedha za kigeni kwa ajili ya utekekelezaji wa mradi wa Uanzishaji wa Kiwanda cha Kutengeneza Mabati inasamehewa.

Ukomo

**3**. Amri hii itafikia ukomo wake tarehe 31 Mei, 2026 kwa kuzingatia kipengele cha 3.3 cha mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Lodhia Steel Industries na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 23 Juni, 2023.

Dodoma, **MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU**
31/12/2024 *Waziri wa Fedha*